



**JAMHURI YA MUUNGANO WA  
TANZANIA  
OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA CHEMBA**

13 Juni, 2022



**TANGAZO LA KOTESHENI / HATI MSAKO**

No. LGA/1.3.6/2021-2022/MFG/NC/01

**KOTESHENI YA KUPATA MZABUNI WA KUVISHA MIFUGO HERENI (EAR TAGS)  
PAMOJA NA UPATIKANAJI**

1. Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, ambapo kwa mujibu wa nukuu hii itajulikana pia kama Mwajiri inatarajia kuvisha hereni za utambuzi ambapo kila Ng'ombe/Punda italipiwa Tshs. 1750/= na kila Mbuzi/Kondoo italipiwa Tshs. 1000/= ambapo gharama hizi zitalipwa na wafugaji wenyewe kwa mifugo yote ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Chemba. Mzabuni atakaepatikana atatakiwa kulipa kwa Halmashauri tshs. 100 kwa kila Ng'ombe/Punda na tshs. 40 kwa kila Mbuzi/Kondoo atakaevishwa hereni.
2. Halmashauri inakaribisha wazabuni wenye sifa zilizotajwa katika kotesheni hii kuomba kazi ya kuvisha hereni Mifugo. Sifa mojawapo awe amesajiliwa na Baraza la Madaktari wa Mifugo Tanzania, awe na leseni ya kufanya kazi hii, awe na Tax clearance na pia awe na mtaji wa kutosha wa kununua hereni na kuendesha zoezi hili.
3. Mwombaji atapewa nyaraka za kotesheni na hakutakuwa na ada ya zabuni katika ofisi ya Manunuzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Chemba.
4. Nyaraka za Kotesheni zitapatikana katika Ofisi ya Manunuzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, S.L.P 830, kuanzia saa 2:00 Asubuhi hadi saa 9:30 Alasiri siku ya Jumatano ya tarehe 15/06/2022 hadi Jumanne ya tarehe 21/06/2022 bila kujumuisha siku za mapumziko na sikukuu za kitaifa.
5. Kotesheni irejeshwe ikiwa imefungwa katika bahasha na ikiwa na nakala halisi (original copy) moja 1 na nakala kivuli (photocopy) moja 1.
6. Mwisho wa kupokea maombi ni Jumanne ya tarehe 21/06/2022, saa 4:00 Asubuhi, ikifuatiwa na ufunguzi utakaofanyika saa 5:00 Asubuhi siku hiyo hiyo katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya. Waombaji/wawakilishi wanaweza kuhudhuria sherehe ya ufunguzi wa kotesheni hizo. Hivyo waombaji wanakaribishwa kuhudhuria ufunguzi huo.
7. Kotesheni zitakazorejeshwa kwa kuchelewa na zitakazotumwa kwa njia ya mtandao, kama vile nukushi na barua pepe hazitofunguliwa na hazitazingatiwa.
8. Bahasha ya nakala halisi (original copy) na bahasha ya nakala kivuli (photocopy) zifungwe ndani ya bahasha moja na bahasha hiyo ifungwe madhubuti (sealed) na juu yake iandikwe anuani hii:

*Katibu wa Bodi ya Zabuni Wilaya, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba,  
S.L.P 830. Chemba – Dodoma.*

Kisha iandikwe jina la kazi iliyoombwa na namba yake (mzabuni).

Siwema Hamoud Jumaa

**MKURUGENZI MTENDAJI (H/W)**

**CHEMBANZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
CHEMBA**